# UMOJA - JARIDA

UNITED NATIONS TANZANIA


## BOTI YA KUBEBA WAGONJWA, "AFYA BORA", YAANZA KAZI RASMI VISIWANI ZANZIBAR


Toleo la 86
Septemba - Oktoba 2019




Boti ya kubeba wagonjwa ni sehemu ya mpango mkubwa zaidi wa msaada wa UNFPA Tanzania kwa Zanzibar ili kuimarisha mifumo yenye ufanisi ya rufaa kwa wajawazito wanaokabiliana na uzazi pingamizi na matatizo mengine ya mimba. **Picha| *UNFPA***

## VIDOKEZO


- Jinsi mradi wa lishe ulivyompa baba asiye na mke fursa nyingine
- Serikali na Umoja wa Mataifa zatoa wito kwa uwekezaji zaidi kwa akina mama na wasichana
- "Kasha la Maajabu" linalotoa nishati safi na kusafisha maji kwa jamii za vijijini
- Tathmini ya sekta ya afya: mafanikio na changamoto


Mvua ilikuwa ikinyesha wakati boti ya kubeba wagonjwa iitwayo *"Afya Bora"* ilipokuwa ikizinduliwa katika bahari inayoizunguka Zanzibar, lakini hali hiyo haikuondoa shamrashamra zilizotawala. Baada ya miaka miwili ya mashauriano na Wizara ya Afya, Mamlaka ya Bahari ya Zanzibar, Idara ya Manunuzi ya Shirika la UNFPA, Copenhagen, boti ya kubeba wagonjwa ya aina yake iliwasili Zanzibar kutoka Sri Lanka na ilikuwa tayari kuanza kazi.

Kwa msaada wa UNFPA Tanzania, na kwa ufadhili wa Serikali ya Kanada kama sehemu ya mradi wa *Afya Bora*,


***Inaendelea Ukurasa wa pili (2)***


## Kauli ya Serikali

***"Msimamo wa Tanzania ni kuunga mkono Umoja wa Mataifa na leo tunasema kwamba Umoja wa Mataifa ni muhimu zaidi sana leo kuliko hata ilivyokuwa wakati wa Vita Baridi...uungaji mkono wetu wa Umoja wa Mataifa ni wa kauli moja na tutapaza sauti zetu kama tulivyofanya miaka ya nyuma dhidi ya wale wanaodhani kwamba ushirikiano wa pande nyingi si muhimu. Kwa hakika ushirikiano huu ni muhimu."***

**Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Mh. Prof. Palamagamba Kabudi, wakati akizungumza wakati wa Kumbukumbu ya Miaka 74 ya Kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa katika Viwanja vya Nyerere jijini Dodoma, Oktoba 24, 2019.**



Boti ya kubeba wagonjwa inayoitwa 'Afya Bora' itasaidia kufanya wajawazito kuwahishwa katika kituo cha afya wakati wa dharura ya kujifungua. **Picha| *UNFPA***

Bi. Jacqueline Mahon, Mwakilishi wa UNFPA nchini Tanzania, alikabidhi rasmi boti hiyo kwa Mh. Hamad Rashid, Waziri wa Afya wa Zanzibar, katika sherehe ya kuvutia. Miongoni mwa waliohudhuria walikuwa Shamata Shaame, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, maofisa wa ngazi za juu kutoka Wizara ya Afya ya Zanzibar na washirika wa maendeleo.

Uzinduzi wa boti ya kubeba wagonjwa ni sehemu ya kampeni ijulikanayo kama Hakikisha Uzazi Salama yenye mikakati iliyotajwa waziwazi ambayo inashuhudia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ikifanya jitihada za kumaliza vifo vinavyozuilika vya akina mama na watoto wachanga.

Boti hiyo ya kubeba wagonjwa itakuwa chombo muhimu sana katika kukabiliana na moja ya sababu kuu za vifo vya akina mama ucheleweshwaji wa upatikanaji wa huduma za dharura ambayo ni sehemu ya msaada mpana zaidi wa UNFPA Tanzania kwa Zanzibar ili kuimarisha mifumo imara ya rufaa, kwa njia ya ardhini na majini.

Boti hiyo ya kubeba wagonjwa, ambayo kituo chake kikuu kitakuwa Chake Chake, Pemba, ambacho ni moja kati ya visiwa vikuu vya Zanzibar, itahudumia visiwa vidogo vya jirani vya Kojani (Wete Magharibi), Makoongwe na Kisiwa Panza (Wilaya ya Mkoani), Fundo, Njao, Uvinje na Kokota. Itatoa msaada wa usafiri kwa akina mama wanaopatwa na dharura wakati wa ujauzito kwa kuwawahisha hadi katika vituo vya afya vya Wilaya ya Wete (Pemba Kaskazini) na Chake Chake na Hospitali ya Mkoani ambazo zote hizi zimejengewa uwezo wa kutoa huduma kamili, dharura ya uzazi pingamizi na matunzo ya watoto wachanga.

Boti hiyo ya wagonjwa itaendeshwa na vikosi maalumu vya KMKM kitengo cha jeshi maji, kuwekewa wahudumu wa afya wenye mafunzo maalumu ya kushughulikia dharura, na kitakuwa na kilo 500 ya vifaa tiba ambapo boti hiyo itapunguza muda wa kusafiri kwa asilimia 50 kulinganisha na ule wa awali.



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

# JINSI MRADI WA LISHE ULIVYOMPA BABA ASIYE NA MKE FURSA NYINGINE




Hussein Saidi akiwa amembeba binti yake muda mfupi baada ya kuwasili katiak Kituo ca Afya cha Ilongero, ambacho kinasaidiwa kupitia mradi wa Boresha Lishe. **Picha|** ***WFP/Catherine Kayombo***

Machoziyanamlengalenga Hussein mwenye umri wa miaka arobaini anapokumbuka siku mkewe alipofariki baada ya kumzaa binti yao, Asha.

Tayari alikuwa anakabiliana na changamoto nyingi. Hussein na mkewe, enzi za uhai wake, walikuwa tayari wazazi kwa mtoto mdogo na huku yeye alikuwa pia akimtunza mama yake asiyeona; hivyo, fikra za kumlea mtoto mchanga peke yake zilimtesa sana.
"Nilitamani kupata msaada," Hussein anasema. "Sikujua nimwendee nani hadi pale nilipokwenda katika kituo cha afya ambako mke wangu alikuwa akipata huduma za kliniki wakati wa ujauzito," anaeleza.

Katika kituo kile cha afya, Hussein alijifunza kuhusu lishe bora na mbinu bora za kulisha watoto wachanga, na vilevile jinsi anavyoweza kufuatilia ukuaji wa Asha, na alipewa chakula kilichoongezewa virutubisho cha kutosha mwezi mmoja kwa ajili ya uji wa Asha.

"Sikuwa na yeyote wa kumwendea, ilinilazimu kutafuta njia bora ya kumtunza mtoto wangu," anasema Hussein. Wakati huohuo ilinipasa kutafuta njia bora ya kumlea mwanangu," alisema Hussein. "Wataalamu wa afya walinipa ushauri wa jinsi ya kumlisha binti yangu na walinielekeza jinsi ya kuandaa mlo kamili," anaeleza.

Kupitia mradi wa Boresha Lishe unaofadhiliwa kwa pamoja na Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Umoja wa Ulaya na Japan WFP inalenga kuimarisha afya ya akina mama na watoto wachanga kwa kuongeza upatikanaji na matumizi ya vyakula bora vya lishe kwa akina mama na watoto, hasa katika siku 1,000 za mwanzo baada ya kuzaliwa.

Kwa kushirikiana na Shirika la Save the Children na asasi za kiraia, Sustainable Environment Management Activity (SEMA) na Research Community and Organization Development Associates (RECODA), takribani akina mama 33,000 wajawazito na wanaonyonyesha na watoto katika mikoa ya Singida na Dodoma ambako mradi unatekeleza wamefikiwa na mradi huo.

WFP pia inashirikiana na Serikali na jamii za mahalia kukabiliana na utapiamlo wa kati na mkali miongoni mwa akina mama na watoto.

# RIPOTI MAALUM I:
# SERIKALI NA UMOJA WA MATAIFA ZATOA WITO KWA UWEKEZAJI ZAIDI KWA AKINA MAMA NA WASICHANA



a) Kupandisha Bendera ya Umoja wa Mataifa kunadhihiisha utayari wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa na kuendeleza tunu zinazoainishwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa. **Picha| *UNCG***

Mnamo Oktoba 24, Umoja wa Mataifa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa pamoja ziliadhimisha kumbukumbu za miaka 74 tangu kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa na hivyo kuimarisha ushirika na ahadi ya kushirikiana zaidi kwa ajili ya utekelezaji wenye mafanikio wa Mpango wa II wa Msaada wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDAP II) na Mpango wa Pili wa Taifa wa Miaka Mitano wa Maendeleo na pia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Kwa mara ya kwanza, Bendera ya Umoja wa Mataifa ilipandishwa katika Viwanja vya Nyerere Jijini Dodoma ambapo Mgeni Rasmi katika hafla hiyo alikuwa Mh. Palamagamba Kabudi, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Bw. Michael Dunford, ambaye ni Kaimu Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa na Mwakilishi wa Nchi wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani, pamoja na Mh. Binilith Mahenge, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, wakuu na wawakilishi wa mashirika ya Umoja wa Mataifa, maofisa wa serikali, wanadiplomasia, wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa, vyombo vya habari na vijana wapatao 250.

Ujumbe wa mwaka huu ulikuwa: "Wanawake na Wasichana wako Mstari wa Mbele Kufikia Malengo ya Dunia" na uliangazia uhusiano kati ya uwezeshaji wanawake na wasichana na ufikiwaji wa Malengo ya Dunia na vipaumbele vya taifa vya maendeleo.

Waziri Kabudi aliipongeza Umoja wa Mataifa kwa kuendeleza ushirika wake na serikali na kusaidia katika utekelezaji wa SDGs hasa Lengo la 5 la Usawa wa Jinsia na alirejea msimamo usioyumba wa Tanzania wa kuendelea kuunga mkono Umoja wa Mataifa.

*Inaendelea Ukurasa wa tano (5)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa Nne (4)*



Wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Chinangali ya Dodoma wakitoa burudani mara baada ya hotuba ya mgeni rasmi. Wanafunzi waliimba shairi linaloonyesha mafanikio katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. **Picha | *UNCG***

"Leo, idadi ya watu duniani ni zaidi ya bilioni 7 na miongoni mwao, watu bilioni 3.7 ni wanawake na wasichana. Licha ya idadi yao na mchango wao mkubwa katika maendeleo ya dunia yetu, wanaendelea kukumbana na magumu mengi kwa sababu ya dosari na matukio ya kihistoria ambayo yalikiuka haki za binadamu. Yote haya yamesababisha wanawake na wasichana kuachwa nyuma katika harakati mbalimbali za kijamii na kiuchumi."

Akizungumza kwa niaba ya Umoja wa Mataifa Tanzania, Bi. Jacqueline Mahon, Mwakilishi wa UNFPA, aliishukuru serikali kwa kuendelea kushirikiana kwa karibu na mashirika ya Umoja wa Mataifa Tanzania katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) akisisitiza kwamba ukosefu wa usawa kati ya wanawake na wanaume hauna budi kutatuliwa ili wanawake na wasichana wapate fursa sawa na kuwezeshwa katika kufikia ndoto na vipawa vyao.

Maadhimisho ya Siku ya Umoja wa Mataifa yaliyofanyika Zanzibar yaliyongozwa na Balozi Seif Ali Iddi, ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Maadhimisho hayo yaliangazia na kuimarisha msaada wa Umoja wa Mataifa kwa wanawake wanojishughulisha na kilimo cha mwani Zanzibar kupitia Programu ya Pamoja ya Zanzibar (ZJP).

Wakati wa maadhimisho hayo, Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa, kwa kutambua na kusaidia kazi ya Umoja Ndiyo Njia Safi Group ambacho ni kikundi cha wanawake wakulima wa mwani kilichoko Bweleo na kinachosaidiwa na ZJP alitangaza kufunga njia tatu za umeme katika kiwanda cha wanawake hao. Huduma hiyo ya umeme iliyofungwa na serikali itakiunganisha kiwanda hicho na mfumo wa umeme ulio wa kutegemewa zaidi, jambo linalomaanisha kwamba wanakikundi wataongeza uwezo wao wa kuchakata bidhaa wanazozalisha.

Akizungumza katika tukio hilo, Balozi Seif Ali Iddi alisema: "Ujumbe wa mwaka huu unaendana na programu za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinazoimarisha haki na ustawi wa wanawake, vijana na wazee, kama inavyoelezwa katika mpango wa maendeleo wa nchi yetu."

*Inaendelea Ukurasa wa sita (6)*

*Kutoka ukurasa wa Tano (5)*




"Leo, kama tunavyofanya kila mwaka, tunahuisha ushirikiano wetu wa muda mrefu kati ya Serikali na watu wa Tanzania, washirika wa maendeleo na Umoja wa Mataifa," Mwakilishi wa UNFPA, Ms. Jacqueline Mahon, alisema kwa niaba ya Umoja wa Mataifa Tanzania wakati wa sherehe za kupandisha Bendera ya Umoja wa Mataifa katika Siku ya Umoja wa Mataifa.

"Kwa wanawake na wasichana wa Tanzania: tafuteni kutimiza ndoto zetu na msiogope au kuona haya kuonyesha ujuzi wenu. Chukueni utawala wa maisha yenu na hatma yenu." **Picha| *UNCG***




"Tanzania inauunga mkono kwa dhati kabisa Umoja wa Mataifa na tunasema kwamba Umoja wa Mataifa ni muhimu zaidi sana sasa kuliko hata wakati wa Vita vya Baridi ... uungaji wetu mkono Umoja wa Mataifa ni kwa msimamo mmoja na tutapaza sauti zetu kama tulivyofanya miaka ya nyuma dhidi ya wale wanaodhani kwamba ushirikano wa pande nyingi si muhimu. Kwa hakika ni muhimu sana." - Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mh. Prof. Palamagamba Kabudi, akisisitiza ushirika wa Serikali na Umoja wa Mataifa. **Picha| *UNCG***

*Inaendelea Ukurasa wa saba (7)*

*Kutoka ukurasa wa Sita (6)*



Kaimu Mratibu wa Umoja wa Mataifa na Mwakilishi wa WFP, Bw. Michael Dunford (kushoto), akikabidhi kibao cha shukrani kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mh. Palamagamba Kabudi (kulia) kumshukuru kwa kuwa mgeni rasmi katika Kumbukumbu za miaka 74 tangu kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa. **Picha| *UNCG***



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mh. Palamagamba Kabudi (aliyeketi katikati) akibadilishana mawazo na Wakuu na Wawakilishi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa (juu) na Wafanyakazi wa UN (chini) ambao walishiriki katika Halfa ya Kupandisha Bendera. **Picha| *UNCG***

***Inaendelea Ukurasa wa nane (8)***

*Kutoka ukurasa wa Saba (7)*



Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kushoto), akitambulishwa kwa Wakuu na Wawakilishi wa Mashirika ya UN mara baada ya kuwasili kwa maadhimisho. **Picha|** ***Imani Nsamila***



Mgeni Rasmi akikabidhi zawadi kwa mwakilishi wa Kikundi cha Umoja Ndio Njia Safi. Kikundi hiki kinachopatikana Bweleo, huchakata bidhaa za sabuni, jamu na mafuta ya kukanda mwili. Wamesaidiwa kuunganishiwa umeme wa njia tatu katika kiwanda chao. Njia hiyo imekiunganisha kiwanda hicho na mkondo mkuu wa umeme wa uhakika, jambo linalomaanisha kwamba kikundi kitaongeza uzalishaji wake. **Picha|*Imani Nsamila***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

# TATHMINI YA SEKTA YA AFYA: MAFANIKIO NA CHANGAMOTO




Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dkt. Zainabu Chaula (wa tatu kutoka kulia), akikabidhi cheti cha shukrani kwa Mwakilishi wa Nchi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dkt. Tigest Ketsela Mengestu (wa pili kulia), kama shukrani kwa shirika hilo kwa mchango wake katika mapitio ya kipindi cha kati cha Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya. **Picha | *WHO***

Kila mwaka, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na washirika wake hukutana ili kupitia maendeleo ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wake wa Kisekta na kubaini vitendo vya kipaumbele vitakavyotekelezwa katika mwaka unaofuatia.

Mwaka huu, mkutano wa Pamoja wa Mwaka wa Mapitio ya Kifundi ya Sekta ya Afya uliandaliwa Jijini Dodoma kutoka Oktoba 8-10, 2019 ili kutathmini mapitio ya kipindi cha kati cha Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya (HSSP IV MTR) na kubaini vipaumbele vya Mpango Mkakati wa V wa Sekta ya Afya unaotarajiwa kuanza kufanya kazi mnamo mwezi Julai, 2020. Katika mkutano huu, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitunukiwa kibao cha kutambuliwa kwa mchango wake katika usaidia mapitio ya kipindi cha kati cha mpango wa sasa wa sekta ya afya.

Dkt. Tigest Ketsela, Mwakilishi wa WHO, na wataalamu wa afya wa WHO walishiriki na kufanya uwasilishaji kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na pia walitoa mapendekezo kuhusu namna Tanzania inavyoweza kufikia malengo yanayohusiana na afya.
Mkutano huo ulipitia Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya ambao utamalizika Juni, 2020 na kutoa mapendekezo kwa Mpango Mkakati wa V wa Sekta ya Afya. Mkutano huo pia ulitunga mapendekezo ya sera kwa mwaka 2020/2021 ambayo yatawasilishwa katika mkutano wa Pamoja wa 20 wa Mwaka wa Sera za Sekta ya Afya mwezi Novemba, 2019.

Mapitio hayo yaliyonyesha kwamba kumekuwa na upigwaji hatua katika ubora wa huduma za afya katika maeneo mengi, kwa kiasi Fulani ikiwa ni kwa sababu ya zoezi la utoaji alama za nyota kwa upimaji, jambo ambalo limewapa wafanyakazi moyo wa kufanya kazi kwa bidii zidi ili kuimarisha ubora wa huduma za afya.
Utendaji wa afya pia unazidi kuimarika kama inavyoonyeshwa na karibu viashiria vyote isipokuwa kwa viwango vya vifo ya mama na mtoto mchanga ambako bado kuna changamoto nyiingi katika upatikanaji wa fedha na rasilimali watu.

Moja ya maeneo ya kukaziwa sana katika Mpango Mkakati wa V wa Sekta ya Afya itakuwa kuhakikisha ushiriki motomoto zaidi wa wanajamii katika ngazi ya jamii kwa lengo la kufikia utoaji huduma za afya kwa wote.

Vipaumbele vingine ni pamoja na kuimarisha utawala, utoaji fedha kwa haki na kwa namna iliyo endelevu, upatikanaji wa rasilimali watu za kutosha, Ufuatiliaji na Tathmini/Taarifa zenye ufanini na tija na upatikanaji wa huduma za Teknolojia, Habari na Mawasiliano na utoaji wa viwango vya juu vya huduma za afya.

# RIPOTI MAALUMU II:
# WAZIRI MKUU AIPONGEZA ILO KWA KUONGOZA UPATIKANAJI WA HAKI YA JAMII NA KAZI ZENYE HADHI KWA MIAKA 100



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa (kushoto kabisa) akitoa pongezi zake kwa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kutimiza miaka 100 na awapongeza kwa mafanikio ya kuhamasisha kazi zenye hadhi nchini Tanzania na kwingineko duniani. **Picha | *ILO***

Mwaka huu ni kumbukumbu ya Miaka 100 ya Shirika la Kazi Duniani (ILO), na mwezi Septemba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mashirika ya wafanyakazi na waajiri, wadau na umma waliungana na ILO jijini Dodoma kwa ajili ya sherehe zake za Karne moja. Mh. Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikuwa ndiye mgeni rasmi.

Miongoni mwa wengine walioshiriki ni pamoja na Mh. Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mh. Maudline Cyrus Castico, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto wa Zanzibar; Bw. Wellington Chibebe, Mkurugenzi wa ILO kwa Afrika ya Mashariki, na maofisa wengine wa ngazi za juu wa serikali.

Waziri Mkuu alizindua kibao maalumu ya Serikali/ILO katika Mji wa Serikali wa Mtumba kama sehemu ya maadhimisho na kuzindua programu ya mafunzo ya uanagenzi ambayo imeshawafikia takribani vijana 46,000 kupitia mafunzo ya ufundi kama vile kushona,

*"Licha ya mafanikio katika soko la ajira na sekta ya kazi kote duniani katika miaka 100 iliyopita, mikakati endelevu inapaswa kubuniwa ili kukabili ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana nchini Tanzania na katika nchi nyingine katika miaka 100 ijayo."*

**Waziri Mkuu Majaliwa akiongea katika maadhimisho ya miaka 100 ya ILO**

***Inaendelea Ukurasa wa kumi na moja (11)***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa Kumi (10)*

umakenika, useremala, umeme, kilimo na uashi.

Akiipongeza ILO kwa kuendelea na juhudi zake za kuisaidia Serikali kuimarisha mazingira bora kazini na kutengeneza nafasi za ajira, na akirudia kusema ahadi ya Serikali kuendelea kuhamasisha ustawi wa maisha ya wafanyakazi na kinga ya kijamii, Waziri Mkuu alisema: "Licha ya mafanikio katika soko la ajira na sekta ya kazi kote duniani katika miaka 100 iliyopita, mikakati endelevu inapaswa kubuniwa ili kukabili ukosefu wa ajira miononi mwa vijana nchini Tanzania na katika nchi nyingine katika miaka 100 ijayo."

Mh. Mhagama alilishukuru Shirika la ILO kwa kusaidia mpango wa utoaji vyeti kwa wafanyakazi wenye ujuzi kupitia programu ya VETA ya Utambuzi wa Mafunzo Kabla ya Kujifunza (RPL), akiongeza kwamba hadi sasa zaidi ya vijana 36,700 wamenufaika na mradi huo.

Bw. Chibebe aliangazia azma ya kuleta haki ya jamii ambayo ndiyo ilisababisha kuzaliwa kwa ILO miaka 100 iliyopita na kwamba bado inaendelea kuwa lengo kuu hata sasa na kwa siku za karibuni zijazo, na kwamba ILO itaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania na washirika wa jamii kuimarisha uhuru wa kuungana pamoja, mijadala ya kijamii na uendelezaji wa ujuzi.

"Tunaendelea kuweka nia ya dhati ya kuhamasisha haki ya jamii, ambayo ni ya msingi kabisa katika kuleta amani ya kudumu kote duniani, na kupigania kuheshimiwa kwa haki za binadamu na za kazi kimataifa," alisema.




Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa (wa pili kushoto), akimpongeza Mkurugenzi wa ILO kwa Afrika Mashariki, Bw. Wellington Chibebe (wa pili kulia) wakati wa maadhimisho ya miaka 100 ya ILO. **Picha | *ILO***

*Inaendelea Ukurasa wa kumi na mbili (12)*

*Kutoka ukurasa wa Kumi na mbili (12)*



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa, akiongoza sherehe upandaji miti kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 100 ya ILO jijini Dodoma. **Picha| *ILO***





Waziri wa Kazi, Ajira, Vijana, Wanawake na Watoto wa Zanzibar, Mh. Maudline Cyrus Castico (kushoto) na Mkurugenzi wa ILO kwa Afrika Mashariki, Bw. Wellington Chibebe (kulia) wakipanda miti kama sehemu ya maadhimisho ya kumbukumbu za miaka 100 ya ILO. **Picha| *ILO***

***Inaendelea Ukurasa wa kumi na tatu (13)***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa Kumi na tatu (13)*



Kikundi cha ngoma za asili kikitumbuiza wakati wa Sherehe za Karne Moja ya ILO. Utumbuizaji wao uliangazia umuhimu wa kutetea haki za kijamii na kazi zenye hadhi, mambo ambayo yanaendana na majukumu ya ILO. **Picha| *ILO***



Wafanyakazi wa ILO wakipiga picha ya pamoja na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Mh. Jenista Mhagama (katikati) baada ya kuzinduliwa kwa kibao cha ILO 100 katika Mji wa Serikali wa Mtumba katika Jiji la Dodoma katika eneo la Ofisi ya Waziri Mkuu. **Picha| *ILO***

# “KASHA LA MAAJABU” LINALOTOA NISHATI SAFI NA KUSAFISHA MAJI KWA JAMII ZA VIJIJINI



‘Off-grid Box’ hii ilifungwa katika Wilaya ya Ikungi, Mkoa wa Singida kupitia msaada wa UNDP. Teknolojia hii inatumia nishati ya jua na kuwawezesha wanachi kupata maji safi na salama pamoja na nishati ya uhakika. **Picha | *UNDP***

Kwa kiasi kikubwa utajiri mkubwa wa Tanzania wa nishati mbadala bado haujaanza kuvunwa, wakati huohuo sehemu kubwa ya watu wake wanaoishi vijijini bado wanategemea kuni kama chanzo chao kikuu cha nishati licha ya kuwa na saa nyingi za kupata jua.

Mambo yako vivyo hivyo kwa upande wa upatikanaji wa maji safi na salama. Ingawa nchi imezungukwa na maziwa makuu manne na bahari na mito mikubwa, ni asilimia ndogo tu ya watu wa vijijini wanaopata maji safi na salama.

Kuvuna rasimali za asili ili kuwapa wakaazi wa vijijini vyanzo safi vya nishati na maji salama kuna uwezekano mkubwa wa kuimarisha viwango vyao vya maisha na afya. Mzigo wa magonjwa yanayoenezwa kwa maji, hasa maeneo ya vijijini, ni mkubwa, huku kuhara, kuharisha na kipindupindu kwa sababu ya kunywa maji yaliyoambikizwa vimelea ni moja ya vyanzo vikubwa vya vifo kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP) linashirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika wilaya tatu za Mkoa wa Mara Bunda, Ikungi na Busega ili kufunga teknolojia ya ‘OffGridBox’ ambao ni mfumo wa vitu vingi kwa pamoja unaotumia nishati ya jua ili kusafisha maji na kusambaza nishati.

Mradi wa ‘Kasha la Maajabu’ utasaidia upatikanaji wa maji

***Inaendelea Ukurasa wa kumi na tano (15)***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa Kumi na nne (14)*

safi na salama na nishati nafuu za maji na nishati safi kwa takribani kaya 4,000 (makadirio ya watu 28,000).

Nishati ya jua inayozalishwa na 'Makasha ya Maajabu' huko Bunda, Ikungi na Busega inaenea hadi katika vijiji sita na visiwa vitatu vilivyo katika Ziwa Victoria. Katika vijiji vyote hivi, wakazi hulazimika ama kununua maji ambayo ni ghali au kutembea zaidi ya kilometa 2 ili kuyateka wenyewe.

Yusuf Masolwa, ambaye ni mwenyekiti wa Kisiwa cha Sozia, anasema: "Kabla ya kufungwa kwa OffGridBox, ilikuwa kawaida kuwa na milipuko ya kipindupindu na kichocho katika kisiwa chetu na ilitupasa kununua lita moja ya maji kwa Sh1,000. Sasa, kwa kutumia kasha hili la maajabu, tunalipa tu Sh200 kwa lita ya maji safi na salama. Kwa hakika haya ni maajabu makubwa!"

Mfumo wa 'OffGridBox' ni kifaa kimoja lakini chenye kutoa masuluhisho mengi na ambacho kinatosha katika kontena la ukubwa a futi 6x6x6 ambalo limefungashiwa vifaa vyote muhimu vinavyohitajika kuzalisha umeme na kusafisha maji. Kasha hilo la maajabu linaweza kujaza umeme hadi vihifadhi umeme 130 vya simu, kusafisha lita 1,000 za maji yanayofaa kunywa na kuunganisha runinga, feni, majokofu na vifaa vinginevyo.

Kasha hili la ajabu, 'OffGridBox', litatoa mchango kwa juhudi za dunia kwamba Tanzania ni sehemu ya Nishati Endelevu kwa Wote na malengo mahususi ya Ajenda 2030.




Tangu Tanzania ipate uhuru, Kisiwa cha Namuguma katika Wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara region, hakijawahi kupata bomba la maji. Lakini baada ya kufungwa kwa 'Off-grid Box', wakazi wa kijiji hicho sasa wanafurahia kupata nishati safi na maji salama. **Picha | *UNDP***

# WARSHA KUHUSU MRADI WA MAJARIBIO YA ZANA YA KIELEKTRONIKI YA MIUNDOMBINU BORA KWA UWEZESHAJI BIASHARA WA UNIDO




Washiriki wakipiga picha ya pamoja wakati wa warsha ya Mradi wa Majaribio wa Miundombinu Bora kwa Uwezeshaji wa Biashara wa UNIDO. Walioketi mstari wa mbele (kutoka kushoto kwenda kulia) ni Bw. Stephen Kargbo, Mwakilishi wa UNIDO; Bw. Leo Lyayuka, Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Viwanda katika Wizara ya Viwanda na Biashara; Bw. Juan Pablo, Meneji Miradi wa UNIDO. **Picha|*UNIDO***

Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara (MITI), liliandaa warsha ya siku mbili iliyofadhiliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo ya Ujerumani ili kufanya mradi wake wa majaribio wa zana za kieletroniki za Miundombinu Bora ili Kuimarisha Biashara (QI4TF).

Lengo la zana hiyo ni kubaini kwa haraka upungufu katika Ubora wa Miundombinu ya Taifa (NQIS) jambo linaloathiri utekelezaji wa Makubaliano ya Uwezeshaji Biashara (TFA) ya Shirika la Biashara Duniani (WTO) ambayo yalianzishwa ili kuongeza kasi ya michakato ya kibiashara ikiwemo usafirishaji, utoaji na upitishaji wa bidhaa. Zana hiyo hutabini upungufu ambao serikali na biashara inayohusika zinapaswa kushughulikia ili kuendana na vifungu fulani vya Makubaliano ya Uwezeshaji Biashara.

Utafiti wa majaribio ya mkono ulifanyika kwa mafanikio mapema mwaka 2019 huko Malawi na Afrika ya Kusini katika uchakataji mazao ya kilimo na sekta ya mafuta muhimu, ambapo matokeo yake ni kupata mwelekeo mzuri wa hatua za ambazo kila nchi inapaswa kuchukua. Baada ya matokeo hayo mazuri kutokana na tathmini ya zana hiyo ya majaribio, UNIDO ilitengeneza zana ya kidijitali ambayo inapunguza michakato inayohusika katika kutumia zana hiyo kutoka miezi 1.5 hadi siku mbili, kwa kutumia jukwaa la mtandaoni.

Zaidi ya wawakilishi 50 kutoka sekta za umma na binafsi kutoka katika mfumo wa miundobinu bora Tanzania na sekta ndogo za migazi na alizeti walishiriki za migazi na alizeti walishiriki katika sekta hiyo ili kufanyia majaribio zana hiyo.

***Inaendelea Ukurasa wa kumi na saba (17)***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa Kumi na sita (16)*

Wakati wa hotuba yake ya uzinduzi, Mwakilishi wa UNIDO, Bw. Stephen Kargbo, alisisitiza kwamba kiini cha mafanikio cha jitihada hii kilikuwa utayari wa MITI kusaidia sekta ya viwanda kuendeleza maendelevu jumuishi na endelevu ya kiviwanda. Aliongeza kwamba zana hiyo itasaidia kubaini upungufu ambao serikali na wadau kutoka sekta binafsi hawana budi kuushughulikia ili kuendana na vifungu vya 4, 5 na 10.3 vya Makubaliano ya TFA.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Viwanda, MITI, Bw. Leo Lyayuka, matokeo ya mradi huo wa majaribio ya zana ni muhimu katika kubaini mahitaji na hatua zinazohitajika kutoka kwa taasisi za umma na wadau ili kuimarisha ushindani katika sekta na kuonyesha mielekeo bayana katika maeneo muhimu kwa utafiti wa siku za baadaye katika mipango iwayo yote ya maendeleo.

Warsha ilihitimisha kwamba awamu ya majaribio ya zana hiyo, ambayo itaandaliwa kwa ajili ya kutumiwa duniani kote imepangwa kuruhusiwa kwa mpangilio hapo Mwaka 2020.

## SENSA YA 2022: KUTUMIA UBUNIFU ILI KUHAKIKISHA KILA MMOJA ANAHESABIWA!



Timu ya kiufundi ya uwandani ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ikitumia tabiti (tablet) kuingiza taarifa mpya za maeneo ya uchukuaji takwimu katika Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma. UNFPA inaisaidia NBS kuandaa ramani za uendeshaji wa Sensa ya Mwaka 2020. **Picha| *UNFPA***

Mara moja kila baada ya muongo mmoja, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huendesha moja ya mazoezi yake yenye changamoto nyingi Sensa ya idadi ya Watu na Makazi. Kazi hii inahitaji kutayarisha mkakati wa kuifikia nchi nzima, kutafuta na kutoa mafunzo kwa wakusanya taarifa, kuendesha kampeni za utoaji elimu kwa umma, kutembelea kila kaya, na kukusanya, kuchambua na kutangaza mzigo mkubwa wa takwimu.

Lengo kuu la kazi hii ni zaidi ya kuhesabu mtu mmojammoja, sensa hutoa taswira ya Tanzania kuna watu wangapi wanaishi nchini, umri, jinsia na mtawanyiko wa makazi yao na cha muhimu zaidi jinsi wanavyoishi, na vilevile tabia nyingine za kiuchumi na kijamii. Sensa ndiyo chanzo kikuu cha takwimu kwa serikali kuu na za mitaa ambazo ni muhimu katika kufanya uamuzi katika utungaji wa sera za maendeleo, mipango na miradi ambayo hatimaye hutumika kuamua mgawanyo wa rasilimali.

*Inaendelea Ukurasa wa kumi na nane (18)*

*Kutoka ukurasa wa Kumi na saba (17)*

Vilevile, takwimu zinazokusanywa huwa na mchango muhimu sana katika kufanya ufuatiliaji wa masuala ya kidemografia ambayo ni muhimu kwa ufuatiliaji na tathmini ya Malengo ya Maendeleo Endelevu, ambayo yanatoa umuhimu mkubwa kabisa katika kutomwacha mtu yeyote nyuma na katika kuwahudumia wale walio pembezoni kwanza.

Hivi sasa ambapo maandalizi ya Sensa ya Tanzania ya mwaka 2022 yamepamba moto, UNFPA Tanzania inaisaidia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (National Bureau of Statistics (NBS) kuandaa ramani kwa ajili ya Sensa ya mwaka 2022.

Kwa mara ya kwanza katika maandalizi ya sense za nchi, teknolojia ya Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (GIS) zitatumika ili kuweka mipaka kwa usahihi wa maeneo ya kuchukua taarifa (enumeration areas (EAs)) maeneo madogomadogo ya kijiografia ambamo kwamo mkusanya taarifa za sense mmoja atapita wakati wa kukusanya data.

Katikati ya mwezi Oktoba, wafanyakazi wa UNFPA pamoja na timu ya kiufundi ya ugani ya NBS walitembelea Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma, na walitumia tabiti (tablet) iliyowekewa mfumo wa GIS ili kutoa taarifa mpya na kuweka mipaka ya EA, na hivyo kujumuisha mipaka mipya iliyoundwa na kuweka alama muhimu kama vile shule, vituo vya afya na maeneo yanakopatikana maji.

Siku iliyofuata wakati wa mkutano wa utoaji taarifa ulioandaliwa na NBS katiak Wilaya ya Bahi, Mkoa wa Dodoma, Naibu Mwakilishi wa UNFPA, Dkt. Wilfred Ochan, alipokea kitabu kinachoonyesha jiografia ya mwaka 2019 ya Wilaya ya Bahi. Kitabu hicho kiliandaliwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa kabisa kama maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kitabu hicho, Dkt. Ochan alirudia kusema kuwa ahadi ya UNFPA ya kuisaidia NBS katika shughuli za maandalizi na katika kusambaza matokeo ya Sensa ya Mwaka 2022 bado ipo, na akisema kwamba utayari mkubwa ulioonyeshwa na serikali wa kuhakikisha kila mmoja anahesabiwa na sauti yake inasikika katika Sensa ya Mwaka 2022 ni jambo muhimu.



Dkt. Wilfred Ochan, Naibu Mwakilkishi wa UNFPA (kushoto), akipokea mipaka ya kijiografia ya 2019 ya Wilaya ya Bahi iliyoandaliwa kutokana na teknolojia ya kisasa kabisa wakati wa kazi ya uandani kama maandalizi ya Sensa ya 2022. **Picha| *UNFPA***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

## SIKU ZA UMOJA WA MATAIFA

**Novemba 25 –** Siku ya Kimataifa ya Kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake

**Novemba 29 -** Siku ya Kimataifa ya Mshikamano na Watu wa Palestina

**Desemba 01 -** Siku ya UKIMWI Duniani

**Desemba 03 -** Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu

**December 05 -** Siku ya Kimataifa ya Wanaojitolea

**Desemba 10 -** Siku ya Haki za Binadamu

**Desemba 18 -** Siku ya Kimataifa ya Wahamiaji

## UMOJA WA MATAIFA MADHUBUTI KWA DUNIA BORA ZAIDI

UNITED NATIONS
TANZANIA


**Ofisi ya Mratibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa**

+255 22 219 5021

info.untz@one.un.org

www.tz.one.un.org



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021